

JKT kuongeza idadi ya ng'ombe

Na Joyce Kasiki, Mafinga

■■■ KIKOSI chä Jeshi la Taifa (JKT) 841 Mafinga kimejiwekea mikakati mbalimbali ikiwemo kuongeza idadi ya ng'ombe wa nyama na maziwa kwa lengo la kutekeleza agizo la Mkuu wa Jeshi hilo la kuvitaka vikosi vya jeshi hilo kuongeza uzaishaji wa mazao mbalimbali ili viweze kujitosheleza kwa chakula. Kaimu Kamanda wa Kikosi 841 Mafinga JKT Luteni Kanali Issa Chalamila aliyasema hayo wakati ya ziara ya waandishi wa habari walio tembelea kikosi hicho ambacho kimejikita katika shughuli za ufugaji na kilimo na uzalishaji mali.

Luteni Kanali Chalamila alisema, idadi ya ng'ombe wa maziwa waliopo sasa ni 120 na wanaokamuliwa ni 20-29 kwa siku huku mpango uliopo ni kuongeza wanaokamuliwa hadi kufikia 100 kwa siku kwa ajili ya kutosheleza kikosi hicho lakini pia nje ya kikosi.

"Kati ya ng'ombe tunaofuga wa maziwa wapo 120 na wanaokamuliwa ni ng'ombe 20-29 kwa siku amba wanatoa lita 200-250 kwa siku ambapo kwa wastani ng'ombe mmoja anatia kwa wastani wa lita tisa kwa siku. Sasa mkakati wetu ni kuwaongeza hadi wafikie 100 wanaokamuliwa kwa siku ili waweze kuzalisha lita za maziwa 1,000 kwa siku," alisema Luteni Kanali Chalamila.

Alisema kikosini hapo wana ng'ombe aina ya chotara na kienyeji amba wo te huboreshwu kuitia watalamu jambo ambalo huchangia kwa kiasi kikubwa mifugo hiyo kutoa kiasi kingi cha maziwa kwa siku.

"Katika kutekeleza azma ya Mkuu wa JKT ya kuelekea katika kujilisha tumejiwekea mikakati mbalimbali

likiwemo kuongeza uzalishaji wa ng'ombe hasa wa maziwa ili kuwa na uzalishaji wa kutosha wa maziwa ili kušambaza na sehemu mbalimbali ndani na nje ya mafinga." alisema.

Vile vile alisema pia wana mpango wa kuongeza uzalishaji wa mbuzi na kondio amba pia wanafugwa katika kikosi hicho.

Kuhusu kilimo alisema, wana ekari 500 ambazo wanalima mahindi, maharage na alizeti ambayo huwasaidia kwa chakula katika kikosi hicho lakini kuiuzia jamii inayozungukua huku akisema kwa mwaka huu wana mpango wa kuanzisha shamba la maparachichi.

Naye mtaalamu wa mifugo Luteni

Francis Breck alisema kutokana na wao kuwa kitivo cha mifugo wamepanga kuongeza shamba la marisho kutoka ekari 22 hadi kufikia 50 ili kukabiliana na uhaba wa chakula cha mifugo hususani katika kipindi cha kiangazi.

Naye kijana wa kujitolea katika Jeshi hilo, Lucy Malema alisema ujuzi wa kilimo na ufugaji walioupata ndani ya Jeshi hilo utawasaidia kwa kiasi kikubwa mara watakapohitimu mafunzo yao. Alisema elimu ya ufugaji waliyoipata watakwendwa kuitumia wakiwa uraiani katika kujijiri wenyewe kwenye suala la ufugaji pamoja na kilimo cha mazao mbalimbali ambayo wamefundishwa shulenii hapo.

KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

Kadi ya pikipiki yenye usajili namba T 177 BSQ ISUZU WIZARD, chassis namba UES73FW4106160, engine namba FW4106160 kwa jina la **RAYA SAID KHALFAN** imepotea. Taarifa imetolewa kituo cha Polisi Jijini Dar es salaam na kupewa jalada namba DAR/MBU/RB/156540/2021. Kwa ye yeyote atakayeokota kadi hiyo anaombwa aipeleke kituo chochote cha polisi kilicho karibu.

KUPOTEA KWA KADI YA GARI

Kadi ya gari yenye usajili namba T 177 BSQ ISUZU WIZARD, chassis namba UES73FW4106160, engine namba FW4106160 kwa jina la **RAYA SAID KHALFAN** imepotea. Taarifa imetolewa kituo cha Polisi Sumbawanga na kupewa jalada namba RUK/SUM/RB/35713/2021. Kwa ye yeyote atakayeokota kadi hiyo anaombwa aipeleke kituo chochote cha polisi kilicho karibu.

TARE
Taar
(ishi
April
Kiwa
yafu

1. G
2. G
3. G
4. G

5. G
6. G

7. GM
8. GM
9. GI

POL